

**HOTUBA YA M. J. MWAFFISI KATIBU MKUU WIZARA YA
MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO KWENYE UFUNGUZI
WA MKUTANO WA KIKAZI WA KUANDAA VIASHIRIA VYA MKATABA
WA KUONDOA AINA ZOTE ZA UBAGUZI DHIDI YA WANAWAKE
KATIKA UKUMBI WA TAASISI YA ELIMU TANZANIA, KIJITONYAMA
TAREHE 29.8.2008**

**Ndugu Mwenyekiti,
Ndugu Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jinsia,
Ndugu Washiriki wa Mkutano ya Ukusanyaji Takwimu,
Ndugu Waandishi wa Habari Mliopo,
Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa kufungua mkutano huu muhimu. Nimefurahishwa na ushiriki wenu ambao umeweza kuwakutanisha washiriki kutoka Wizara za Serikali, Maafisa wa Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya zake, Vyama vya Wafanyakazi na Mashirika ya Kidini. Mikutano kama hii ni hatua mojawapo inayowezesha watumishi na wafanyakazi kutoka katika maeneo mbalimbali kufahamiana na kubadilishana uzoefu.

Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru UNFPA kwa kuwezesha mkutano huu muhimu wa kikazi kufanyika, ambao una jukumu kubwa la kuandaa viashiria vitakavyowezesha kupima na kupata taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake.

Ndugu Washiriki,

Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake ulizinduliwa mwaka 1979 na kuanza kutekelezwa mwaka 1981. Tanzania iliusaini mwaka 1985, ikaridhia mwaka 1986 na taarifa ya awali ikapelekwa mwaka 1987. Jukumu la uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa Mkataba huu ni la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara zetu mbili za Muungano ambazo ni Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto Zanzibar.

Ndugu Washiriki,

Taarifa ya Nchi ya Kwanza ilipelekwa mwaka 1990 na ya Pili na ya Tatu zilipelekwa kwa pamoja mwaka 1998. Taarifa za Nne, Tano na Sita ziliwasilishwa na kutetewa kwenye Kamati ya utetezi Umoja wa Mataifa mwaka huu Julai 2008. Taarifa inayofuata inatakiwa ipelekwe mwaka 2010. Kwa mantiki hiyo ninyi kama wataalam wa kutoka sekta mbalimbali ni chachu ya kufanikisha uandaaji wa viashiria vitakavyowezesha kupata taarifa na takwimu sahihi za utekelezaji wa Mkataba huo. Serikali pia inalo jukumu la kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinawafikia raia wake wote wake kwa waume ili wawe na uelewa wa hatua ambazo zimefikwa kuhusu suala hili. Vile vile inawajibika kuwashirikisha katika utayarishaji wa taarifa hizo. Ndio maana tupo hapa leo kuandaa viashiria vya ukusanyaji taarifa ili muweze kutoa utaalamu na uzoefu wenu katika kuandaa viashiria hivyo.

Ndugu Washiriki,

Mkataba huu hutambuliwa kama Sheria ya Haki za Wanawake na unaitaka kila nchi Mwanachama kuchukua hatua zinazofaa kuhakikisha kuwa Maendeleo kamili ya wanawake yanapatikana katika nyanja zote za maendeleo. Masuala ya Haki za Wanawake yamesisitizwa pia katika Mkutano Mkuu wa Nne wa Umoja wa Mataifa wa Wanawake uliofanyika Beijing China mwaka 1995, Beijing +5 na Beijing +10. Vilevile na Serikali yetu imekuwa ikihimiza maendeleo ya Wanawake na Jinsia katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa lengo la kuleta usawa wa jinsia. Hivyo ni matumaini yangu kuwa Mkutano huu utafanya kazi hii kwa makini na kutoka na viashiria vitakavyoweza kupata taarifa na takwimu sahihi kwa manufaa ya taifa letu.

Ndugu Washiriki,

Sasa napenda kutamka rasmi kuwa mkutano huu wa Kuandaa Viashiria vya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake umefunguliwa.

Asanteni kwa kunisikiza.